Edit with WPS Office

UUNDAJI WA MANENO

Kuunda maneno ni kitendo cha kuzalisha maneno mapya katika lugha. Lugha yoyote ile huhitaji maneno mapya ili kuweza kukidhi mahitaji ya mawasiliano.

Katika lugha ya Kiswahili kuna maneno ambayo hayawezi kugawika zaidi kisarufi bila kupoteza maana mfano : baba, mama, Sali, kaka, huzuni, safi n.k . Maneno hayo yaani yasiyogawika zaidi kisarufi hujulikana kama mofimu.

Pia katika lugha ya Kiswahili yapo maneno mengine ambayo yamejengwa kwa kupachikwa au kuongezwa vipashio ambapo bila vipashio hivyo neno haliwezi kujitosheleza kimaana. **Mfano:**

Mzizi	**Neno lilitokana na kupachikwa vipashio**
-lim-	amelima (a-me-lim-a)
-toto	mtoto (m-toto)
-chez-	anacheza (a-na-chez-a)

Katika mifano hiyo hapo juu vipashio vilivyoongezwa ili kuunda neno lenye maana huitwa mofimu.

Mofimu ni kipashio kidogo kabisa cha kiisimu chenye maana ya kisarufi au kileksika .

"Kipashio kidogo " kina maana ya umbo la neno au umbo katika neno lisiloweza kugawanywa katika sehemu nyingine ndogo zaidi. Hivyo basi udogo wa kipashio sio wa kiumbo bali ni kwamba hakuna mgawanyo wa kisarufi unaoweza kufanyika au kufanywa zaidi.

Mofimu zenye maana ya kileksika ni mofimu ambazo haziambatanishwi na kipashio chochote mfano baba, Mungu, fikiri, bora n.k

Mofimu zenye maana ya kisarufi ni mofimu zinazoambatanishwa na mofimu nyingine katika uundaji wa maneno. Mofimu hizo huambatanishwa kwenye mzizi wa neno

Mfano

Ki-atu
m-toto
tu-ta-som-a
m-gonjwa

Hivyo neno au maneno huweza kuundwa na mofimu moja tu au zaidi.

Mfano:

NENO	IDADI YA MOFIMU
Samehe	Moja (ambayo ni samehe)
Mkulima	Nne(ambazo ni m-ku-lim-a)
Walipigana	Tano (ambazo ni wa-li-pig-an-a)
shangazi	Moja (ambayo ni shangazi)

AINA ZA MOFIMU

Kuna aina mbili za mofimu ambazo ni mofimu huru na mofimu tegemezi.

MOFIMU HURU

Ni mofimu inayoweza kusimama peke yake na kuleta maana kamili. AU

Ni mofimu inayoweza kusimama peke yake na kuweza kutumiwa katika tungo bila kuwa na kiambishi chochote.

Mofimu huru zina hadhi ya neno kwasababu hujitosheleza kimaana hivyo mofimu huru huweza kuwa ni aina yoyote ya neno kama vile;

Nomino Asha, mama, kaka, Anna, babu n.k

Edit with WPS Office

Vitenzi samehe, tafiti,jibu, lia n.k
Vivumishi zuri, baya, fupi, kile n.k
Viwakilishi Yule, sisi, wewe, mimi n.k
Vielezi kabisa, haraka, sana, vizuri n.k
Viunganishi hata, lakini,sababu, na n.k
Vihusishi kwa, katika, kutoka n.k

MOFIMU TEGEMEZI

Ni mofimu ambayo haiwezi kusimama peke yake na kuleta maana. AU
Ni mofimu zinazofungamana na mofimu nyingine na zinapotumika hutegemeana ili kueleza dhana iliyokusudiwa.
Mofimu tegemezi hupachikwa katika mzizi (kiini) wa neno. Mzizi wa neno ni ile sehemu ya neno ambayo hubeba maana ya msingi ya neno na huwa haibadiliki mfano -chez-, -som-, -pik-, -lim- n.k

Mfano

Mofimu tegemezi	Mzizi	Mofimu tegemezi	Neno
A – li –ye –	pig-	w-a	Aliyepigwa
M-	toto		Mtoto
Wa-si-o-	som-	a	Wasiosoma
Tu – na – vyo-	imb-	a	Tunavyoimba

DHIMA ZA MOFIMU

i. Kuzalisha maneno ya lugha inayohusika

Hii hufanywa kwa kupachika vipashio au mofimu tegemezi kwenye mzizi(kiini) wa neno yaani kwa kutumia mzizi wa neno maneno mbalimbali huweza kupatikana au kuzalishwa kwa kubadili mofimu tegemezi. Kwa mfano kutokana na mzizi **–lim-** tunapata maneno kama vile anayelima, analimwa, analimika, analimisha, analimia, analimishwa, n.k

ii. Kudokeza nafsi katika kitenzi

Mofimu huonyesha nafsi katika kitenzi, mofimu hizo huwekwa kabla ya mzizi wa neno.

Mfano

Nafsi		Mofimu	Neno
I	Umoja	Ni-	**Ni**naimba
	Wingi	Tu-	**Tu**naimba
II	Umoja	U-	**U**naimba
	Wingi	M –	**M**naimba
III	Umoja	A –	**A**naimba
	Wingi	Wa-	**Wa**naimba

iii. Kuonesha umoja na wingi katika nomino na vivumishi:

Edit with WPS Office

Mofimu huweza kuwekwa kabla ya mzizi wa nomino au vivumishi ili kuonyesha umoja na wingi (idadi).

Mfano

Umoja	**Wingi**
M-toto	Wa-toto
U-gonjwa	Ma-gonjwa
M-baya	Wa-baya

iv. Kuonesha njeo (wakati) katika kitenzi

Njeo ni kategoria ya kisarufi ambayo huwakilisha muda au wakati tendo linatendeka, lilitendeka au litatendeka au halikutendeka. Hivyo mofimu ya njeo huwekwa kabla ya mzizi wa neno (kitenzi) ili kuonyesha wakati wa kutendeka kwa tendo.

Mfano

A**na**lala	(-na- wakati uliopo)
A**li**lala	(-li- wakati uliopita)
A**ta**lala	(-ta- wakati ujao)

v. Kuonesha hali mbalimbali katika kitenzi.

Mofimu zinazoonesha hali katika kitenzi huwekwa kabla ya mzizi wa neno na huonesha au hudokeza kama kitendo kinaendelea kufanyika au hufanyika mara kwa mara au kama kimemalizika kufanyika. Hali hizo ni kama zifuatazo;

a) Hali ya kuendelea kwa tendo. Huwakilishwa na mofimu –na-
   Mfano; a**na**soma, a**na**cheka, a**na**pigwa, a**nak**imbia, n.k
b) Hali timilifu. Huwakilishwa na mofimu -me-
   Mfano; a**me**lala, wa**me**chapwa, tu**me**kuja, ni**me**kimbia, n.k
c) Hali ya mazoea. Huwakilishwa na mofimu –hu-
   Mfano; **hu**cheka, **hu**pika, **hu**lima, **hu**kimbia, n.k
d) Hali ya masharti. Huwakilishwa na mofimu –ki-, -nge-, -ngeli-, -ngali-
   Mfano; A**ki**ja, a**nge**soma, a**ngeli**tibiwa, a**ngali**cheza, n.k

vi. Kuonesha uyakinishi na ukanushi katika kitenzi.

Mofimu zina kazi ya kuonesha kama tendo limefanyika au halijafanyika.

Mfano

Uyakinishi	**Ukanushi**
Analia	**ha**lii
Nitakuja	**Si**takuja
Umelala	**Hu**kulala

vii. Hudokeza urejeshi wa mtenda, mtendwa au mtendewa katika kitenzi.

Mofimu ya urejeshi wa mtenda huwakilisha yule anayetenda tendo, mofimu ya urejeshi wa mtendwa huwakilisha mtu au kitu kilichoathiriwa na kitendo moja kwa moja yaani kitu kilichopokea tendo, mofimu ya urejeshi wa mtendewa huwakilisha mtu au kitu kisichoathiriwa na kitendo moja kwa moja yaani wale ambao kitendo hufanywa kwa niaba yao.

Mfano

Ana**ye**sema	-ye- mofimu ya urejeshi wa mtenda

Edit with WPS Office

Wana**m**soma -m- mofimu ya urejeshi wa mtendwa
Ali**ni**imbia -ni- mofimu ya urejeshi wa mtendewa

viii. Kuonesha kauli mbalimbali za tendo (vitenzi)
Mofimu huweza kuwekwa baada ya mzizi wa neno (kitenzi) ili kuwakilisha kauli mbalimbali katika lugha. Baadhi ya kauli hizo ni kama vile;

- Kauli ya kutenda (mofimu –a) mfano; anachez-**a**, wanali-**a**, tunakul-**a,** n.k
- Kauli ya kutendwa (mofimu –w-) mfano; amepig-**w**-a, wanachez-**w**-a, ninalim-**w**-a,n.k
- Kauli ya kutendeka (mofimu –ik- na –ek-) mfano anasom-**ek**-a, wanachez-**ek**-a, tunapig-**ik**-a, n.k
- Kauli ya kutendesha (mofimu –ish-, -esh-, -z-,) mfano som-**esh**-a, anapig-**ish**-a, li-**z**-a, n.k
- Kauli ya kutendana (mofimu –an-) mfano wanaimb-**an**-a, tumelim-**an**-a, mmesom-**an**-a, n.k

ix. Huonesha ukubwa wa nomino. Mofimu huweza kupachikwa kabla ya mzizi wa nomino ili kuonyesha dhana ya ukubwa,

Mfano

Nyumba **ju**mba au **ma**jumba
Mtu **ji**tu au **ma**jitu
Kisu **ji**su

x. Huonesha udogo wa nomino. Mofimu huweza kupachikwa kabla ya mzizi wa nomino kuonyesha hali ya udogo au kudunishwa kwa kitu (nomino)

Mfano

Nyumba **ki**nyumba
Mfalme **ki**falme
Gari **ki**gari
Msichana **ki**sichana

KUUNDA MANENO KWA KUTUMIA UAMBISHAJI

Uambishaji ni upachikaji wa mofimu katika mzizi (kiini) wa neno ambao huonesha upatanisho wa kisarufi. AU
Ni njia ya kuunda maneno kwa kupachika mofimu tegemezi kabla na baada ya mzizi wa neno.
Katika lugha ya Kiswahili uambishaji huweza kufanywa kabla na baada ya mzizi wa neno. **Kwa mfano mzizi –som-** huweza kupachikwa mofimu kabla na baada na kuunda maneno kama anaye**soma**, ali**som**wa, wame**som**eka, unam**som**ea, mna**som**ana, n.k
Mofimu zinazopachikwa kabla na baada ya mzizi wa neno huitwa <u>viambishi.</u>

<u>VIAMBISHI</u>

Viambishi ni mofimu zinazowekwa kwenye mzizi wa neno na kukamilisha muundo wa neno.
Katika lugha ya Kiswahili viambishi huweza kuambikwa au kupachikwa kabla na baada ya mzizi wa neno.

AINA ZA VIAMBISHI

Kuna aina kuu mbili za viambishi katika lugha ya Kiswahili ambazo ni

Edit with WPS Office

a. Viambishi awali
b. Viambishi tamati

A. **VIAMBISHI AWALI**

Ni viambishi ambavyo huwekwa au hupachikwa kabla ya mzizi wa neno. Viambishi awali katika neno huweza kuwa kimoja au zaidi.

Mfano

Neno	**Viambishi awali**
Mtu	m-
Walipona	Wa-li-
Kilichovunjika	Ki-li-cho-
Aliyempigia	a-li-ye-m-

Viambishi awali vipo vya aina mbalimbali kama ifuatavyo;

- Viambishi Ngeli na idadi
  Hivi hupachikwa kabla ya mzizi wa nomino na vivumishi ili kudokeza umoja na wingi au idadi.
  Mfano

Umoja	**Wingi**
Mtundu	**Wa**tundu
Mgomba	**Mi**gomba
Kiatu	**Vi**atu

- Viambishi vipatanishi
  Ni viambishi awali ambavyo hufanya kazi ya kuonesha nafsi katika kitenzi.
  Mfano

Nafsi	**Viambishi awali**	**Neno**
I Umoja	Ni-	**Ni**nasema
Wingi	Tu-	**Tu**nasema
II Umoja	U-	**U**nasema
Wingi	M-	**M**nasema
III Umoja	A –	**A**nasema
Wingi	Wa -	**Wa**nasema

Viambishi awali vya ukanushi
Ni viambishi awali ambavyo huwekwa kabla ya mzizi wa kitenzi ili kuwakilisha hali ya ukanushi.

Mfano

Ninasoma	**Si**somi
Unasoma	**Hu**somi
Anasoma	**Ha**somi
Soma	U**si**some

Edit with WPS Office

Viambishi vya njeo

Ni viambishi ambavyo huwekwa kabla ya mzizi wa kitenzi ili kuwakilisha wakati ambapo tendo lilitendeka au halikutendeka. Katika lugha ya Kiswahili kuna njeo zifuatazo;

Wakati uliopo

Huwakilishwa na kiambishi –na- katika uyakinishi na kiambishi –i- katika ukanushi ambapo kiambishi –i- hutokea kama kiambishi tamati.

Mfano

Ni**na**imba	Siimb**i**
Wa**na**cheza	Hawachez**i**
Tu**na**lima	Hatulim**i**

Wakati uliopita

Huwakilishwa na kiambishi –li- katika uyakinishi na kiambishi –ku- katika ukanushi

Mfano

Ni**li**fagia	si**ku**fagia
Wa**li**lia	hawa**ku**lia
Tu**li**lala	hatu**ku**lala

Wakati ujao

Huwakilishwa na kiambishi –ta- katika uyakinishi na ukanushi.

Mfano

M**ta**cheza	Ham**ta**cheza
Ni**ta**pika	Si**ta**pika
U**ta**lia	Hau**ta**lia

Viambishi vya hali

Hali ni kipengele cha kisarufi ambacho katika kitenzi hutumika kuonyesha muda au kipindi maalum ambacho tendo lilifanyika.

Katika lugha ya Kiswahili hali hizo huwakilishwa kama ifuatavyo;

Hali ya mazoea

Huwakilishwa na kiambishi –na-

Mfano

Ni**na**imba
Tu**na**pika
Wa**na**kula

Hali timilifu

Huwakilishwa na kiambishi –me-

Mfano

A**me**lala
Wa**me**ondoka
Tu**me**pigwa

Hali ya mazoea

Huwakilishwa na kiambishi –hu-

Mfano

Hukimbia
Husoma
Hufaulu

Hali ya masharti

Edit with WPS Office

Huwakilishwa na viambishi –ki-, -nge-, -ngeli- na –ngali-.

Mfano

A**ki**shinda
A**nge**shinda
A**ngeli**shinda
A**ngali**shinda

Viambishi rejeshi vya mtenda, mtendwa au mtendewa

Viambishi hivi hutaja mtenda yaani aliyefanya tendo, mtendwa yaani mtu au kitu kilichoathiriwa na kitendo moja kwa moja na mtendewa yaani kitu au mtu asiyeathiriwa na tendo moja kwa moja au ambao tendo hufanywa kwa niaba yao.

Viambishi vya mtendwa na mtendewa huwa havitokei kwa pamoja katika kitenzi kimoja.

Mfano

Ali**ni**piga -ni- kiambishi cha urejeshi wa mtendwa
Uli**o**enea -o- kiambishi cha urejeshi wa mtenda
Wali**tu**andikia -tu- kiambishi cha urejeshi wa watendewa

B.VIAMBISHI TAMATI

Ni viambishi ambavyo huwekwa baada ya mzizi wa neno.

Mfano

Neno	Viambishi tamati
Limia	-i-a
Chezesha	-esh-a
Wanachezewa	-ew-a
Soma	-a
Taifishika	-ik-a

Viambishi tamati hufanya kazi ya kudokeza kauli mbalimbali za vitenzi.

Mifano

Kauli ya kutenda; huwakilishwa na kiambishi tamati –a.

Mfano: lima, chez**a**, li**a**, omb**a**,n.k

Kauli ya kutendana; huwakilishwa na kiambishi tamati –an-

Mfano: som**an**a, pig**an**a, lili**an**a, n.k

Kauli ya kutendeka; huwakilishwa na viambishi tamati –ik-, -ek-,-lek-, -lik-, -k-,

Mfano: zal**ik**a, som**ek**a, ng'ol**ek**a, epu**k**a n.k

Kauli ya kutendewa; huwakilishwa na viambishi tamati –iw-, -ew-

Mfano: limi**w**a, som**ew**a, piki**w**a, lili**w**a, n.k

DHIMA ZA UAMBISHAJI

1.Kuzalisha maneno ya lugha inayohusika

Hii hufanywa kwa kupachika viambishi kwenye mzizi(kiini) wa neno yaani kwa kutumia mzizi wa neno maneno mbalimbali huweza kupatikana au kuzalishwa kwa kubadili viambishi. Kwa mfano kutokana na mzizi –toto maneno kama vile mtoto, kitoto,utoto n.k huweza kuundwa.

2.Kudokeza nafsi katika kitenzi

Uambishaji huonyesha nafsi katika kitenzi ambapo viambishi vya nafsi huwekwa kabla

Edit with WPS Office

ya mzizi wa neno.

Mfano

Anasoma	**a-** kiambishi cha nafsi ya III umoja
Unaimba	**u-** kiambishi cha nafsi ya II umoja
Tumelala	**tu-** kiambishi cha nafsi ya I wingi

3.Kuonesha umoja na wingi katika nomino na vivumishi:

Uambishaji huonyesha umoja na wingi wa nomino na vivumishi au idadi ya nomino na vivumishi.

Mfano

Umoja	**Wingi**
M-zazi	Wa-zazi
U-gonjwa	Ma-gonjwa
M-zuri	Wa-zuri

4. Kuonesha njeo (wakati) katika kitenzi

Uambishaji huonesha wakati wa kutendeka kwa tendo yaani kama tendo linafanyika wakati huo, lilishafanyika au litafanyika.

Mfano

A**na**cheza	(-na- kiambishi cha wakati uliopo)
A**li**fikisha	(-li- kiambishi cha wakati uliopita)
A**ta**ondoka	(-ta- kiambishi cha wakati ujao)

5.Kuonesha hali mbalimbali katika kitenzi.

Uambishaji huonesha au hudokeza hali ya kitendo (vitenzi) yaani kama kitendo kinaendelea kufanyika au hufanyika mara kwa mara au kama kimemalizika kufanyika. Hali hizo ni kama zifuatazo;

e) Hali ya kuendelea kwa tendo. Huwakilishwa na kiambishi –na-
   Mfano; a**na**somwa, a**na**chekelea, a**na**pigwa, a**nak**imbizwa, n.k
f) Hali timilifu. Huwakilishwa na kiambishi -me-
   Mfano; a**me**lazwa, wa**me**chapwa, tu**me**kuja, ni**me**kimbia, n.k
g) Hali ya mazoea. Huwakilishwa na kiambishi –hu-
   Mfano; **hu**cheka, **hu**pika, **hu**lima, **hu**kimbia, n.k
h) Hali ya masharti. Huwakilishwa na viambishi –ki-, -nge-, -ngeli-, -ngali-
   Mfano; A**ki**ja, a**nge**soma, a**ngeli**tibiwa, a**ngali**cheza, n.k

6.Kuonesha uyakinishi na ukanushi katika kitenzi.

Uambishaji huonesha kama tendo limefanyika au halijafanyika.

Mfano

Uyakinishi	**Ukanushi**
Anakula	**ha**li
Nitafika	**Si**tafika
Umepata	**Hu**kupata

7.Hudokeza urejeshi wa mtenda, mtendwa au mtendewa katika kitenzi.

Uambishaji hudokeza urejeshi wa mtenda yaani yule anayetenda tendo, mtendwa

Edit with WPS Office

yaani mtu au kitu kilichoathiriwa na kitendo moja kwa moja yaani kitu kilichopokea tendo na mtendewa yaani mtu au kitu kisichoathiriwa na kitendo moja kwa moja(wale ambao kitendo hufanywa kwa niaba yao).

Mfano

Ana**ye**lima -ye- kiambishi cha urejeshi wa mtenda
Wana**m**cheka -m- kiambishi cha urejeshi wa mtendwa
Ali**ni**kimbia -ni- kiambishi cha urejeshi wa mtendewa

8.Kuonesha kauli mbalimbali za tendo (vitenzi)

mfano

- Kauli ya kutenda (kiambishi –a) mfano; anachez-**a**, wanali-**a**, tunakul-**a,** n.k
- Kauli ya kutendwa (kiambishi –w-) mfano; amepig-**w**-a, wanachez-**w-**a, ninalim-**w**-a,n.k
- Kauli ya kutendeka (viambishi –ik- na –ek-) mfano anasom-**ek**-a, wanachez-**ek**-a, tunapig-**ik**-a, n.k
- Kauli ya kutendesha (viambishi –ish-, -esh-, -z-,) mfano som-**esh**-a, anapig-**ish**-a, li-**z**-a, n.k
- Kauli ya kutendana (viambishi –an-) mfano wanaimb-**an**-a, tumelim-**an**-a, mmesom-**an**-a, n.k

KUUNDA MANENO KWA NJIA YA MNYUMBULIKO

Mnyumbuliko ni njia ya kuunda maneno kwa kuongeza viambishi katika mzizi wa neno. Unyumbuaji wa maneno hufanywa kwa kuongeza viambishi tamati katika mzizi wa neno hivyo basi viambishi tamati vikipachikwa kwenye mzizi wa neno, neno au maneno hayo huwa yamenyumbuliwa.

Mfano

Neno	Mzizi (kiini)	Maneno ya mnyumbuliko
Penda	Pend-	Pendwa, pendeka,pendana,pendon.k
Imba	Imb-	Imbika, imbisha, imbishwa, imbia, imbana, n.k
Lima	Lim-	Limia, limika, limisha, limia, limiwa, n.k
Ruka	Ruk-	Rukwa, rukia, rukisha, rukiwa, n.k

Maneno mbalimbali katika lugha huweza kuundwa kwa kunyumbua aina mbalimbali za maneno kama vile

a) Nomino

Baadhi ya nomino hasa nomino za jumla huweza kupachikwa viambishi tamati na kuunda vielezi. Mara nyingi vielezi hivyo huwa ni vya mahali.

Mfano

Nomino	Vielezi
Uwanja	Uwanja**ni**
Msikiti	Msikiti**ni**
Chumba	Chumba**ni**

Edit with WPS Office

Vilevile nomino huweza kunyumbuliwa au kuongezwa baada ya mzizi wa neno na kuunda vitenzi.

Mfano

Nomino	**Vitenzi**
Taifa	Taifisha, taifishana, taifishwa, taifishika, n.k
Chuki	Chukizwa, chukiza, chukia, chukiana, n.k
Furaha	Furahishwa, furahishana,furahia,furahiana, n.k

b) Vivumishi

Vivumishi pia huweza kunyumbuliwa na kuunda vitenzi

Mfano

Vivumishi	**Vitenzi**
Chafu	Chafuka, chafuana,chafuliwa,chafua,n.k
Nene	Nenepa,nenepeana, nenepeshwa, n.k
Fupi	Fupisha, fupika, fupishia,fupishana, n.k

c) Vielezi

Baadhi ya vielezi huweza kunyumbuliwa na kuunda vitenzi.

Mfano

Vielezi	**Vitenzi**
Haraka	Harakishwa , harakisha, harakishana, n.k
Karibu	Karibia, karibishwa, karibiana, karibishana, n.k

d) Vitenzi

Vitenzi huweza kunyumbuliwa kwa kuongezewa viambishi vya mnyumbuliko na kuunda vitenzi vipya ambavyo huonyesha kauli mbalimbali za tendo au vitenzi kama vile kauli ya kutenda, kauli ya kutendwa, kauli ya kutendana n.k

Mfano

Kauli ya kutenda pig-**a**, som-**a**, pik-**a,** li-**a,** n.k
Kauli yakutendwa elez-**w**-a, pig-**w**-a, chot-**w-**a, pendez-**w**-a, n.k
Kauli ya kutendeka vut-**ik-**a, end-**ek**-a, twa-**lik-**a, zo-**lek**-a, ibu-**k-**a, n.k
Kauli ya kutendana ping-**an**-a, o-**an-**a, saidi-**an**-a, harib-**ian-**a, hukum-**ian**-a,
Kauli ya kutendesha it-**ish-**a, nyw-**esh**-a, pit-**ish-**a, ku-**z-**a, n.k
Kauli ya kutendewa suk-**iw-**a, zo-**lew-**a, som-**ew**-a, tup-**iw**-a, n.k
Kauli ya kutendea chez-**e-**a, lim-**i-**a, som-**e**-a, pig-**i**-a, n.k

DHIMA YA MNYUMBULIKO

a) Huongeza msamiati wa lugha

Kwa kunyumbua mzizi wa maneno tunapata maneno mbalimbali **mfano** kwa kutumia mzizi **pend-** tunapata maneno kama pendwa, pendeka, pendelewa, pendana, n.k

b) Huzalisha kauli mbalimbali za vitendo

Kutokana na mnyumbuliko kauli mbalimbali za vitenzi huzalishwa katika lugha ya

Edit with WPS Office

Kiswahili. Kama vile kauli ya kutenda, kutendwa, kutendea n.k

c) Hupanua maana mbalimbali za maneno

Mnyumbuliko husaidia kupanua maana ya neno yaani neno kupata maana nyingine baada ya kunyumbuliwa

Mfano

Kata kutenganisha kitu kwa kutumia kitu au kifaa chenye makali kama vile kisu

Kat-i-a tenganisha kitu kwa niaba ya mtu mwingine

MATUMIZI YA LUGHA KATIKA MIKTADHA MBALIMBALI

Matumizi ya lugha ni hali au namna ya kutumia lugha kulingana na mila, desturi na utaratibu wa jamii.

Mila, desturi na taratibu za jamii husika humsaidia mtumiaji wa lugha kutumia lugha ipasavyo kutegemeana na uhusiano uliopo baina ya wazungumzaji, mahali mazungumzo yanapofanyika,je mazungumzo yanahusu nini na lengo la mazungumzo hayo ni nini.

Hivyo matumizi yoyote ya lugha hutegemea au huzingatia mambo makuu manne (4) yafuatayo;

i.Uhusiano baina ya wazungumzaji (wahusika)

ii.Muktadha au mazingira

iii.Mada ya mazungumzo

iv.Madhumuni au lengo la mazungumzo

Uhusiano baina ya wazungumzaji

Lugha inayozungumzwa hutegemea sana uhusiano uliopo baina ya mzungumzaji na msikilizaji ambapo uhusiano wao huo huwaongoza katika kuteua mtindo wa lugha utakaotumika katika mazungumzo yao. Uhusiano unaweza kuwa kati ya Mwalimu na mwanafunzi, mzazi na mototo, rafiki na rafiki, mfanyakazi na mwajiri, n.k

Mfano: a)**Uhusiano kati ya Mwalimu na mwanafunzi**

Mwanafunzi: Shikamo Mwalimu

Mwalimu: Marahaba

b**) uhusiano kati ya watu wa rika moja (rafiki na rafiki**)

Juma: Mambo vipi mshikaji

John: Aisee ni poa tu. Niaje?

Muktadha au mazingira

Mazingira mara nyingi ndiyo hutawala uzungumzaji wa mhusika kwani mzungumzaji huwa na uhuru wa kutumia lugha apendavyo kutegemeana na mazingira aliyopo. Kwa mfano inaweza kuwa ni mazingira ya mahakamani, hospitalini, nyumbani, mtaani, n.k

Mfano

Kunywa moja mara tatu - hospitalini

Dogo kazingua sana - mtaani

Umehukumiwa miaka mitatu jela na kulipa faini - mahakamani

Mada ya mazungumzo

Mada ya mazungumzo hutawala usemaji na jinsi ya kuzungumza. Hivyo mada ya

Edit with WPS Office

mazungumzo humwongoza mzungumzaji katika uteuzi wa maneno ya kutumia. Kutegemeana na mada ya mazungumzo tunaweza kupata lugha ya kibiashara, kisiasa, kisheria, n.k

Madhumuni au lengo la mazungumzo

Mzungumzaji yeyote huwa na lengo la kufikisha ujumbe fulani anapozungumza hivyo mzungumzaji hujitahidi kutoa ufafanuzi wa yale anayosema ili kufikia lengo alilokusudia kwa kuzingatia mada, uhusiano uliopo baina yao na hata mazingira aliyopo.

Hivyo basi muktadha, uhusiano baina ya wazungumzaji, mada ya mazungumzo na madhumuni ya mazungumzo ni vipengele muhimu vinavyomuongoza mzungumzaji yeyote yule kuteua maneno na tungo atakazotumia kulingana na mazingira aliyopo.

REJESTA

Rejesta ni mtindo wa lugha unaotumika katika mazingira maalum kama vile sokoni, hotelini, mahakamani, hospitalini, n.k.
Mtindo wa lugha huweza kubadilika au kutumika kutegemeana na mahali mzungumzaji alipo, shughuli anayoifanya, uhusiano wa wahusika na hata mada ya mazungumzo.
Hivyo basi rejesta ni muhimu kwa ajili ya kukidhi haja ya mawasiliano katika mazingira fulani maalumu.

Mfano: Hotelini au mgahawani
Mhudumu: nani mkia?
Mteja: Mimi

AINA ZA REJESTA

Kuna aina mbalimbali za rejesta kulingana na mahali au shughuli inayofanywa na wahusika. Baadhi ya aina hizo ni;

i. **Rejesta za mitaani**
Ni mtindo wa lugha unaotumiwa na kundi Fulani la watu ambapo lugha hiyo hueleweka kwa wazungumzaji wenyewe. Lugha hiyo huweza kudumu kwa muda mfupi na kufifia au kupotea.
Mfano
Mzungumzaji 1: Niaje mshikaji mbona pande Fulani hukuibuka?
Mzungumzaji 2: Acha tu msela wangu maza alizingua

ii. **Rejesta zahospitalini**
Ni lugha inayotumiwa na wahudumu, madaktari, manesi na wagonjwa hospitalini. Lugha hii mara nyingi huwa ni ya upole, mkato na yenye kutia matumaini aidha kwa mgonjwa au ndugu zake.**mfano:** kutwa mara tatu, mbili mara moja, leta choo, n.k

iii. **Rejesta za mahakamani**
Ni mtindo wa lugha unaotumika mahakamani. Maneno kama vile mshtakiwa, mtuhumiwa, hakimu, kesi namba, wazee wa baraza, n.k hutumika
Mfano

Edit with WPS Office

Mshtakiwa: Mheshimiwa hakimu naomba usinipe adhabu kali kwani nina mke na watoto wadogo wananitegemea.

iv. **Rejesta za hotelini**

Ni mtindo wa lugha unaotumika hotelini. Mara nyingi katika mtindo huu mzungumzaji hutumia lugha ya mkato ili kuokoa muda wa kutoa huduma.

Mfano:

Mhudumu: Nani wali maharage?
Mteja: Mimi
Mhudumu: Mkia wapi?
Mteja: Hapa.

DHIMA ZA REJESTA

i) Hutumika kama kitambulisho cha wazungumzaji
Rejesta hutumika kama kitambulisho kwani mtindo wa lugha unaotumika humtambulisha mzungumzaji na shughuli anayoifanyak mfano kama ni mchungaji, Mwalimu, mwanasiasa, daktari, n.k

ii) Hutumika kurahisisha mawasiliano
Hii ni kutokana na matumizi ya lugha ya mkato ambayo husaidia kutoa ujumbe uliokusudiwa kwa kifupi hivyo kuokoa muda na kuwahudumia watu wengi kwa muda mfupi au wakati mmoja. Kwa mfano hospitalini, hotelini, n.k

iii)Husaidia katika kukuza lugha
kutokana na matumizi ya rejesta mbalimbali lugha husika huweza kuunda msamiati wake kwani baadhi ya maneno huwezakusanifishwa na kuingizwa katika msamiati wa lugha husika, hivyo lugha hukua kutokana na kitendo hicho. Mfano maneno kama dingi, shangingi, kibaka ni maneno yaliyotumiwa kama rejesta lakini baadae yalisanifishwa na kuingizwa katika kamusi.

iv)Huficha jambo kwa watu wasiohusika
Rejesta huwasidia watu walio katika kundi moja tu kuelewa kile kinachozungumziwa kwani kama si mhusika huwezi kuelewa mzungumzaji anamaanisha nini.
Kwa mfano kama si daktari huwezi kuelewa lugha wanayoitumia kama vile
Bs – kupima malaria
Stool – kupima choo

v) Hutumika katika kupamba lugha.
Hii ni kutokana na kutumia lugha ya mkato na msamiati unaovutia hivyo humvutia msikilizaji kusikiliza tofauti na lugha ya kawaida hivyo rejesta hupamba lugha.

vi) Hutumika kupunguza ukali wa maneno
Hii ni kwa sababu rejesta hujumuisha pia matumizi ya tafsida ambayo husaidia kupunguza ukali wa maneno. Mfano amejifungua badala ya kuzaa.

MISIMU (SIMO)

Misimu ni maneno yasiyo sanifu yanayozushwa na kikundi cha watu wachache wenye utamaduni mmoja ili kuelezea mahusiano yao kama kikundi au kuhusu jamii kubwa ambamo vikundi hivyo vinaishi katika kipindi Fulani

Edit with WPS Office

cha maisha au wakati.
Maneno yanayozushwa huweza kudumu kwa muda Fulani na kisha kupotea (kutoweka) na yanayodumu huingizwa kwenye msamiati wa lugha husika baada ya kusanifiwa.

CHANZO CHA MISIMU

Misimu katika lugha huweza kutokana na

i) Mabadiliko ya kihistoria yanayoikumba jamii katika nyakati mbalimbali. Mabadiliko hayo yanaweza kutokana na maendeleo ya sayansi na teknlojia, siasa, uchumi, n.k.

ii) Hali ya utani miongoni mwa watu mbalimbali. Misimu ya aina hii hubeba kebehi,
dhihaka, kejeli au kusifu kusiko kwa kawaida.

AINA ZA MISIMU

Kuna aina kuu tatu (3) za misimu ambazo ni;

i. Misimu ya pekee
ii. Misimu ya kitarafa
iii. Misimu zagao

Misimu ya pekee

Misimu hii huelezea uhusiano wa kikundi kimoja cha watu wenye utamaduni mmoja. Huitwa misimu ya pekee kwa sababu hujulikana pale ilipozukia tu na sio nje ya eneo hilo hivyo eneo la matumizi la misimu hii huwa ni dogo (finyu). Kwa mfano misimu ya pekee huweza kutumiwa na wanafunzi wa shule moja, wafanyakazi wa ofisi moja, wachezaji wa timu moja, n.k

Misimu ya kitarafa

Ni aina ya misimu ambayo huweza kutumika katika kata, tarafa, wilaya, mkoa au kanda hivyo aina hii ya misimu huchukua eneo pana kidogo kimatumizi. Ueneaji wa misimu ya kitarafa huchangiwa na muingiliano wa watu katika shughuli zao mbalimbali za kila siku mfano katika biashara, michezo, dini, n.k

Misimu zagao

Ni aina ya misimu ambayo huenea karibu nchi nzima na wakati mwingine huweza kuvuka mipaka ya nchi.
Misimu zagao huweza kutumika katika vyombo vya habari kama vile magazeti, redio na televisheni. Baadhi ya misimu zagao huweza kusanifiwa na kuingizwa katika msamiati wa lugha husika. Mfano wa misimu zagao ni mpambe, ngangari, hapa kazi tu, buzi, bwege, n.k

SIFA ZA MISIMU

i. Huzuka na kutoweka. Hii ni kutokana na mabadiliko mbalimbali ya kihistoria yanayoikumba jamii katika vipindi mbalimbali. Kwa mfano kipindi cha mfumo wa vyama vingi maneno kama wapambe, ngangari, ngunguri, hapa kazi tu, wapambe, n.k
ii. Ni lugha isiyo sanifu. Kwa sababu huanzishwa na watu kutokana na hisia zinazowapata kwa wakati huo (Fulani) na huwa ni nje ya msamiati wa lugha husika.

Edit with WPS Office

iii. Ni lugha ya mafumbo. Misimu hufahamika kwa watu wachache walio katika kikundi kimoja.
iv. Ina chumvi nyingi. Hii ni kwa sababu maneno ya misimu huongezewa chumvi nyingi hivyo hubeba hisia za kejeli, kebehi, sifa zisizo za kawaida, n.k.
v. Hupendwa na watu wengi. Hii hutokana na kuwa misimu ina sifa ya kuchekesha na huongeza mvuto katika lugha.

NJIA ZIUNDAZO MISIMU

i. Njia ya kufupisha maneno. Neno huweza kufupishwa kwa makusudi na kuwa misimu. **Mfano** : Inahu – inahusu
Utajiju – utajijua
Disco –discontinued
Bro – brother

ii. Njia ya kutohoa kutoka lugha za kigeni.
Misimu inaweza kuundwa kwa kuchukua neno (maneno) kutoka katika lugha moja na kuyaingiza katika lugha nyingine. ambapo neno hilo lililotoholewa huweza kubadika katika namna ya uandishi au utamkaji au likabaki kama lilivyochukuliwa kutoka katika lugha husika.
Mifano
Sizi –cease
Demu –dame
Antisosho –antisocial
Fegi –fag
Faza – father

iii. Njia ya kutumia sitiari.
Sitiari ni mlinganisho wa ufanano wa umbo, rangi, kimo, kazi, n.k. hivyo kuna baadhi ya misimu hutokana na kuwepo kwa mfanano wa kiumbo, kazi, rangi, kimo, n.k
Mfano:
Amevaa chupa –badala ya suruali nyembamba.

iv. Njia ya kutumia tanakali sauti. Misimu huweza kuundwa kutokana na mlio wa kitu unaosikikika.
Mfano : Neno malapa limetokana na sauti isikikayo pindi mtu aliyevaa kandambili
anapotembea.

v. Njia ya kubadili maana ya msingi ya neno.
Mfano: Maneno kama nimemfia, nimemzimia yana maanisha nimempenda

SABABU ZA KUTUMIA MISIMU

i. Kufanya mazungumzo yawe ya siri ili wasiohusika wasielewe. Mfano nafunga ofisi au tuamshe popo maana yake tuondoke au naondoka au tutoroke
ii. Hupunguza uzito au ukali wa jambo wakati wa kulitamka. Misimu hufanya mambo mazito yaonekane ya kawaida na mepesi.
iii. Kudhani ndiyo ujuzi wa lugha. Baadhi ya watumiaji wa misimu hudhani ni sifa mojawapo ya kujua lugha wanapoyatumia maneno hayo.**Mfano** Soo, msala –tatizo

Edit with WPS Office

DHIMA ZA MISIMU

i. Kukuza lugha. Misimu husaidia katika kukuza lugha kwani baadhi ya misimu inayoota mizizi huweza kusanifiwa na kuingizwa kwenye msamiati wa lugha hivyo kuongeza msamiati wa lugha.**mfano** daladala, magendo, marupurupu n.k

ii. Kupamba lugha. Kutokana na sifa ya kuchekesha misimu hutumika kupamba lughakwani watu hupenda kuitumia ili kunogesha mazungumzo yao.

iii. Kufupisha mawasiliano ili kueleweka kwa haraka. Maneno ya misimu huwa ni mafupi hivyo humsaidia mzungumzaji kufupisha maelezo na kueleweka kwa haraka**. Mfano** neno daladala

iv. Kupunguza ukali wa maneno. Misimu husaidia kupunguza ukali wa maneno wakati wa kuzungumza**.mfano** kula vitu, kula mzigo – kufanya mapenzi

v. Kuhifadhi historia ya jamii. Kutokana na mabadiliko ya kihistoria yanayoikumba jamii misimu huzuka ili kuelezea mabadiliko hayo hivyo kama misimu ikiendelea kutumika hutunza historia ya jamii**.**

Mfano:

Muda mfupi baada ya kupata uhuru- uhuru na kazi, uhuru na umojan.k

Wakati wa azimio la Arusha – unyonyaji, kupe, makabaila, mabepari, n.k

Vita vya kagera – fashisti iddi, nduli iddi Amini, n.k

Mfumo wa vyama vingi – hapa kazi tu, ngangari, wapambe, ngunguri, n.k

Edit with WPS Office

Edit with WPS Office

Edit with WPS Office